(imesahihishwa 01/19)

U.S. Citizenship and Immigration Services

# Maswali ya Masomo ya Siasa (Historia na Serikali) kwa Mtihani wa Uraia

Maswali na majibu 100 ya masomo ya siasa (historia na serikali) kwa mtihani wa uraia yameorodheshwa hapa chini. Mtihani wa masomo ya siasa ni mtihani wa kuongea na afisa wa USCIS atauliza mwombaji hadi 10 kati ya maswali 100 ya masomo ya siasa. Mwombaji lazima ajibu 6 kati ya maswali 10 kwa usahihi ili kupita sehemu ya masomo ya siasa ya mtihani wa uraia.

Katika mtihani wa uraia, baadhi ya majibu yanaweza kubadilika kwa sababu ya uchaguzi au uteuzi. Unaposomea mtihani, hakikisha kuwa unajua majibu ya sasa kwa maswali haya. Jibu maswali haya na jina la afisa ambaye anatumika wakati wa mahojiano yako ya kustahiki na USCIS. Afisa wa USCIS hawezi kukubali jibu lisilo sahihi.

**Hata ingawa USCIS inajua kwamba kunaweza kuwa na majibu sahihi ya zaidi ya moja, waombaji wanahimizwa kujibu maswali ya masomo ya siasa kwa kutumia majibu yalipewa hapa chini.**

## SERIKALI YA MAREKANI

### A: Kanuni za Demokrasia ya Marekani

1. **Ni sheria ipi kuu ya nchi?**
   - *katiba*
2. **Katiba inafanya nini?**
   - *inaunda serikali*
   - *inafafanua serikali*
   - *inalinda haki za msingi za Wamarekani*
3. **Wazo la serikali binafsi liko katika maneno matatu ya kwanza ya katiba. Maneno haya ni yapi?**
   - *Sisi Watu*
4. **Marekebisho ni nini?**
   - *badilisho (kwa Katiba)*
   - nyongeza *(kwa Katiba)*
5. **Tunaitaje marekebisho kumi za kwanza katika Katiba?**
   - *Muswada wa Haki*
6. **Ni nini haki <u>moja</u> au uhuru ilioko kwenye Marekebisho ya Kwanza?***
   - *kuongea*
   - *dini*
   - *mkutano*
   - *vyombo vya habari*
   - *malalamishi kwa serikali*
7. **Katiba ina marekebisho mangapi?**
   - *ishirini na saba (27)*
8. **Tamko la Uhuru lilifanya nini?**
   - *lilitangaza uhuru wetu (Kotoka Uingereza)*
   - *lilitamka uhuru wetu (kutoka Uingereza)*
   - *lilisema kwamba Marekani ni huru (kutoka Uingereza)*

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

9. **Ni haki zipi <u>mbili</u> zilizoko kwenye Tamko la Uhuru?**
   - *maisha*
   - *uhuru*
   - *kutafuta furaha*

10. **Ni nini uhuru wa dini?**
   - *Unaweza kuishi maisha ya kidini au kuishi bila kidini.*

11. **Mfumo wa kiuchumi Marekani ni**
   - *uchumi wa kibepari*
   - *uchumi wa soko*

12. **Ni nini "utawala wa sheria"?**
   - *Kila mtu lazima afuate sheria.*
   - *Viongozi lazima watii sheria.*
   - *Serikali lazima itii sheria.*
   - *Hakuna aliye juu ya sheria.*

**<u>B: Mfumo wa Serikali</u>**

13. **Taja tawi moja au sehemu ya serikali.***
   - *Bunge*
   - *baraza la watunga sheria*
   - *Rais*
   - *mtendaji*
   - *koti*
   - *mahakama*

14. **Ni nini kinachozuia tawi <u>moja</u> la serikali kuwa na mamlaka zaidi?**
   - *ukaguzi na usawazishaji*
   - *kutenganisha mamlaka*

15. **Ni nani anayesimamia tawi la mtendaji?**
   - *Rais*

16. **Ni nani anayetengeneza sheria za shirikisho?**
   - *Bunge*
   - *Seneti na Baraza (la Wawakilishi)*
   - *Watunga sheria (marekani au kitaifa)*

17. **Sehemu <u>mbili</u> za Bunge la Marekani ni zipi?***
   - *baraza la Seneti na Nyumba (ya Wawakilishi)*

18. **Maseneta wangapi wa Marekani wapo??**
   - *mia moja (100)*

19. **Tunamchagua Seneta wa Marekani kwa miaka mingapi?** ▪ *sita (6)*

20. **Ni nani <u>mmoja</u> wa Masenta wa Marekani wa Jimbo lako sasa?* -** *Roy Blunt, Josh Howley*
   - *Majibu yatatofautiana. [Wakazi wa Wilaya ya Columbia na wakazi wa maeneo ya Marekani wanapaswa kujibu kuwa D.C. (au eneo ambalo mwombaji anaishi) haina Maseneta wa Marekani.]*

21. **Baraza la Wawakilishi lina wanachama wangapi wa kupiga kura**
   - *mia nne na thelathini na tano (435)*

22. **Tunamchagua Mwakilishi wa Marekani kwa miaka mingapi?** ▪ *mbili (2)*

23. **Taja Mwakilishi wako wa Marekani.** – *Ann Wagner or Cori Bush*
   - *majibu yatatofautiana. [Wakazi wa maeneo yenye Wajumbe wasiopiga kura au Makamishna Wakazi wanaweza kutoa jina la Mjumbe huyo au Kamishna. Pia inayokubalika ni maelezo kwamba eneo hilo halina Wawakilishi (wapiga kura) katika Bunge.]*

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

**24. Seneta wa Marekani anawakilisha nani?**
- *watu wote wa jimbo hilo*

**25. Kwa nini baadhi ya Majimbo yana Wawakilishi zaidi kuliko Majimbo mengine?**
- (kwa sababu ya) idadi ya watu wa jimbo hilo
- (kwa sababu) wana watu wengi zaidi
- (kwa sababu) baadhi ya majimbo yana watu wengi zaidi

**26. Tunamchagua Rais kwa miaka mingapi?**
- *nne (4)*

**27. Ni mwezi gani ambapo tunampigia kura Rais?***
- *Novemba*

**28. Jina la Rais wa Marekani sasa ni nani?***
- *Joseph Biden*
- *Joe Biden*
- *Biden*

**29. Jina la Makamu wa Rais wa Marekani sasa ni nani?**
- *Kamala Harris*
- *Harris*

**30. Kama Rais hawezi tena kuhudumu, nani anakuwa Rais?**
- *Makamu wa Rais*

**31. Kama Rais na Makamu wa Rais hawawezi tena kuhudumu, nani anakuwa Rais?**
- *Spika wa Bunge*

**32. Amri Jeshi Mkuu wa Majeshi ni nani??**
- *Rais*

**33. Ni nani anayesaini miswada ili kuwa sheria?**
- *Rais*

**34. Nani anakataa miswada?**
- *Rais*

**35. Baraza la Mawaziri la Rais linafanya nini?**
- *linamshauri Rais*

**36. Je, nafasi mbili za Baraza la Mawaziri ni zipi?**
- katibu wa Kilimo
- katibu wa Biashara
- katibu wa Ulinzi
- katibu wa Elimu
- katibu wa Nishati
- katibu wa Huduma za Afya na Binadamu
- katibu wa Usalama wa Nchi
- katibu wa Nyumba na Maendeleo ya Miji
- katibu wa Mambo ya Ndani
- katibu wa Kazi
- katibu wa Jimbo
- katibu wa Usafirishaji
- katibu wa Hazina
- katibu wa Mambo ya Mashujaa
- katibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali
- katibu Makamu wa Rais

**37. Tawi la mahakama linafanya nini?**

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

- linakagua sheria
- linaeleza sheria
- linasuluhisha migogoro (kutokubaliana)
- linaamua ikiwa sheria inaenda kinyume cha Katiba

**38. Mahakama ya juu zaidi nchini Marekani ni ipi?**
- *Mahakama Kuu*

**39. Ni Majaji wangapi walioko katika Mahakama Kuu?**
- *tisa (9)*

**40. Jaji Mkuu wa Marekani sasa ni nani?**
- *John Roberts (John G. Roberts, Jr.)*

**41. Chini ya Katiba yetu, baadhi ya mamlaka ni ya serikali ya shirikisho. Je, ni mamlaka gani moja ya serikali ya shirikisho?**
- *kuchapisha pesa*
- *kutangaza vita*
- *kuunda jeshi*
- *mikataba*

**42. Chini ya Katiba yetu, baadhi ya mamlaka ni ya majimbo. Je, ni mamlaka gani moja ya majimbo?**
- kutoa masomo na elimu
- kutoa ulinzi (polisi)
- kutoa usalama (idara za moto)
- kupeana leseni ya uendeshaji
- kuidhinisha ugavi wa eneo na matumizi ya ardhi

**43. Gavana wa jimbo lako sasa ni nani?**
- *Mike Parson*
- *majibu yatatofautiana. [Wakazi wa Wilaya ya Columbia wanapaswa kujibu kwamba D.C. haina Gavana.]*

**44. Mji mkuu wa jimbo lako ni nini?*** - *Jefferson City*
- *majibu yatatofautiana. [Wakazi wa Wilaya ya Columbia wanapaswa kujibu kwamba D.C. sio jimbo na haina mji mkuu. Wakaazi wa maeneo ya Marekani wanapaswa kutaja mji mkuu wa eneo hilo.]*

**45. Je, vyama vikuu viwili vya siasa nchini Marekani ni vipi?***
- *Kidemokrasia na Ripablikan*

**46. . Chama cha siasa cha Rais wa sasa ni kipi?**
- Chama cha Ripablikan

**47. Jina la Spika wa Baraza la Wawakilishi sasa ni nani?**
- *Nancy Pelosi*

## C: Haki na Wajibu

**48. Kuna marekebisho manne ya Katiba kuhusu nani anaweza kupiga kura. Elezea moja yao.**
- Raia wa miaka kumi na minane (18) na zaidi (wanaweza kupiga kura).
- Hautakikani kulipa (kodi ya kura) kupiga kura.
- Raia yeyote anaweza kupiga kura. (Wanawake na wanaume wanaweza kupiga kura.)
- Raia wa kiume wa kabila lolote (anaweza kupiga kura).

**49. Ni jukumu gani moja ambalo ni la raia wa Marekani tu?***
- kutumika kwenye baraza la wahukum
- kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho

**50. Taja haki moja ambalo ni la raia wa Marekani tu.**
- *kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho*
- *kugombea ofisi ya shirikisho*

**51. Ni haki zipi mbili za kila mtu anayeishi Marekani?**

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

- *uhuru wa kujieleza*
- *uhuru wa kuuongea*
- *uhuru wa kukusanyika*
- *uhuru wa kulalamika kwa serikali*
- *uhuru wa dini*
- *haki ya kubeba silaha*

**52. Tunaonyesha uaminifu wetu kwa nani tunaposema Ahadi ya Utii?**
- *kwa nchi ya Marekani*
- *kwa bendera*

**53. Ni ahadi gani <u>moja</u> unayotoa unapokuwa raia wa Marekani?**
- *kata uaminifu kwa nchi zingine*
- *tetea katiba na sheria za Marekani*
- *tii sheria za Marekani*
- *tumika katika jeshi la Marekani (ikiwa inahitajika)*
- *tumika (fanya kazi muhimu ya) taifa (ikiwa inahitajika)*
- *kuwa mtiifu kwa Marekani*

**54. Wananchi wanatakiwa kuwa na umri gani wa kumpigia kura Rais?***
- *Kumi na nane (18) au zaidi*

**55. Ni njia zipi <u>mbili</u> ambazo Wamarekani wanaweza kushiriki katika demokrasia yao?**
- *Kupiga kura*
- *kujiunga na chama cha siasa*
- *kusaidia katika kampeni*
- *kujiunga na kikundi cha kiraia*
- *kujiunga na kikundi cha jamii*
- *kutoa maoni yako kwa afisa aliyechaguliwa juu ya suala*
- *kupigia simu Maseneta na Wawakilishi*
- *kuunga mkono hadharani au kupinga suala au sera*
- *kugombea madaraka*
- *kuandikia gazeti*

**56. Ni lini siku ya mwisho unayoweza kutuma fomu zako za kodi ya mapato kwa shirikisho?***
- *Aprili 15*

**57. Ni lini wanaume wote lazima wawe wamejiandikisha kwa Huduma ya Kuchagua?**
- *akifikisha umri wa miaka kumi na nane (18)*
- *kati ya kumi na nane (18) na ishirini na sita (26)*

## HISTORIA YA MAREKANI

### <u>A: Kipindi cha Ukoloni na Uhuru</u>

**58. Je, ni sababu gani <u>moja</u> ya wakoloni kuja Marekani?**
- *uhuru*
- *uhuru wa kisiasa*
- *uhuru wa kidini*
- *nafasi za kujijenga kiuchumi*
- *kuweza kuweka dini zao*
- *kuepuka mateso*

**59. Ni nani walioishi Marekani kabla ya Wazungu kuwasili?**
- *Wamerikani Wahindi*
- *Wamarekani Wenyeji*

**60. Ni kikundi gani la watu lililopelekwa Marekani na kuuzwa kama watumwa?**

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

- *Waafrika*
- *Watu kutoka Afrika*

**61. Ni kwa nini wakoloni walipigana na Waingereza?**

- *kwa sababu ya kodi kubwa (ushuru bila uwakilishi)*
- *kwa sababu jeshi la Uingereza lilikaa katika nyumba zao (kama bweni, uwekaji)*
- *kwa sababu hawakuwa na serikali la kujitegemea*

**62. Ni nani aliyeandika Tamko la Uhuru?**

- *(Thomas) Jefferson*

**63. Tamko la Uhuru lilipitishwa lini?**

- *Julai 4, 1776*

**64. Kulikuwa na majimbo 13 ya mwanzo. Taja tatu.**

- *New Hampshire*
- *Massachusetts*
- *Rhode Island*
- *Connecticut*
- *New York*
- *New Jersey*
- *Pennsylvania*
- *Delaware*
- *Maryland*
- *Virginia*
- *North Carolina*
- *South Carolina*
- *Georgia*

**65. Nini kilitokea kwenye Mkataba wa Katiba?**

- *Katiba iliandikwa.*
- *Baba waanzilishi waliandika Katiba.*

**66. Katiba iliandikwa lini?**

- *1787*

**67. Hati za Shirikisho ziliunga mkono Katiba ya Marekani. Taja mmoja wa waandishi.**

- *(James) Madison*
- *(Alexander) Hamilton*
- *John) Jay*
- *Publius*

**68. Ni kitu gani kimoja ambacho Benjamin Franklin ni maarufu kwa?**

- *mwanadiplomasia wa Marekani*
- *mwanachama mzee zaidi wa Mkutano wa Katiba*
- *Mkuu wa kwanza wa Shirika la Posta la Marekani*
- *mwandishi wa "Poor Richard's Almanac"*
- *alianzisha maktaba ya kwanza ya kutumiwa bila malipo*

**69. Ni nani "Baba wa Nchi Yetu"**

- *(George) Washington*

**70. Ni nani aliyekua Rais wa kwanza?***

- *(George) Washington*

## B: Miaka za 1800

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

**71. Ni eneo gani ambayo Marekani ilinunua kutoka kwa Ufaransa mwaka wa 1803?**

- *Eneo la Louisiana*
- *Louisiana*

**72. Taja vita moja iliyopiganwa na Marekani miaka za 1800.**

- *Vita vya 1812*
- Vita vya *Mexico-Amerika*
- *Vita vya wenyewe kwa wenyewe*
- *Vita vya Wahispania-Wamarekani*

**73. Taja vita vya Marekani kati ya Kaskazini na Kusini.**

- *Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe*
- *Vita kati ya Majimbo*

**74. Taja tatizo moja lililosababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe.**

- *utumwa*
- *sababu za kiekonomia*
- *haki za majimbo*

**75. Ni kitu gani kimoja muhimu ambacho Abraham Lincoln alifanya?***

- *aliwapa uhuru watumwa (Tangazo la Uhuru)*
- *aliokoa (au kuhifadhi) Muungano*
- *aliongoza Marekani wakati wa Vita vya wenyewe kwa wenyewe*

**76. Tangazo la Uhuru lilifanya nini?**

- *liliwaweka huru watumwa*
- *liliwaweka huru watumwa katika Shirikisho*
- *liliwaweka huru watumwa katika majimbo ya Shirikisho*
- *liliwaweka huru watumwa katika majimbo mengi ya Kusini*

**77. Susan B. Anthony alifanya nini?**

- *alipigania haki za wanawake*
- *alipigania haki za raia*

## C: Historia ya Marekani ya Hivi karibuni na Habari Ziingine Muhimu za Kihistoria

**78. Taja vita moja iliyopiganiwa na Marekani katika miaka za 1900.***

- *Vita vya I Duniani*
- *Vita vya II Duniani*
- *Vita vya Korea*
- *Vita vya Vietnam*
- *Vita vya Ghuba (Uajemi)*

**79. Ni nani alikuwa Rais wakati wa Vita vya I Duniani?**

- *(Woodrow) Wilson*

**80. Ni nani alikuwa Rais wakati wa Majonzi Kuu na Vita vya II Duniani?**

- *(Franklin) Roosevelt*

**81. Ni nani waliopigana na Marekani katika Vita vya II Duniani?**

- *Japani, Ujeremani, na Italia*

82. Kabla ya kuwa Rais, Eisenhower alikuwa jenerali. Alikuwa kwa vita gani?

- *Vita vya II Duniani*

**83. Wakati wa Vita Baridi, je, wasiwasi kuu ya Marekani ilikuwa nini??**

- *Ukomyuministi*

**84. Ni vuguvugu gani zilizojaribu kumaliza ubaguzi wa rangi?**

- *(vuguvugu) ya haki za kiraia*

**85. Martin Luther King, Jr. alifanya nini?***

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

- *haki za kiraia*
- *alifanya kazi ya usawa kwa Wamarekani wote*

**86. Ni tukio gani kubwa lililotokea Septemba 11, 2001, nchini Marekani**

- *Magaidi waliishambulia Marekani.*

**87. Taja kabila moja la Wamarekani Wahindi nchini Marekani.**

*[Maafisa wa USCIS watapatiwa orodha ya makabila ya Wamarekani Wahindi yanayotambuliwa na shirikisho.]*

- *Cherokee*
- *Navajo*
- *Sioux*
- *Chippewa*
- *Choctaw*
- *Pueblo*
- *Apache*
- *Iroquois*
- *Creek*
- *Blackfeet*
- *Seminole*
- *Cheyenne*
- *Arawak*
- *Shawnee*
- *Mohegan*
- *Huron*
- *Oneida*
- *Lakota*
- *Crow*
- *Teton*
- *Hopi*
- *Inuit*

## MCHANGANYIKO WA MASOMO YA URAIA

### A: Jiografia

**88. Taja moja ya mito miwili mirefu zaidi nchini Marekani.**

- *(Mto wa) Missouri*
- *(Mto wa) Mississippi*

**89. Bahari gani liko katika Pwani ya Magharibi ya Marekani?**

- *(Bahari la) Pasifiki*

**90. Bahari gani liko katika Pwani ya Mashariki ya Marekani?**

- *(Bahari la) Atlantiki*

**91. Taja moja ya eneo la Marekani.**

- *Puerto Rico*
- *U.S. Virgin Islands*
- *American Samoa*
- *Northern Mariana Islands*
- *Guam*

**92. Taja jimbo moja ambalo linapakana na Canada.**

- *Maine*
- *New Hampshire*
- *Vermont*

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.

- *New York*
- *Pennsylvania*
- *Ohio*
- *Michigan*
- *Minnesota*
- *Dakota Kaskazini*
- *Montana*
- *Idaho*
- *Washington*
- *Alaska*

**93. Taja jimbo moja ambalo linapakana na Mexico.**

- *California*
- *Arizona*
- *New Mexico*
- *Texas*

**94. Mji mkuu wa Marekani ni ipi?***

- *Washington, D.C.*

**95. Sanamu ya uhuru liko wapi?**

- *New York (Harbor)*
- *Kisiwa cha Liberty Island*

*[Pia yanayokubaliwa ni New Jersey, karibu na New York City, na kwa (Mto wa) Hudson.]*

**B: Ishara**

**96. Ni kwanini bendera ina malani?**

- *kwa sababu kulikuwa na makoloni 13 mwanzoni*
- *kwa sababu malaini yanawakilisha makoloni ya mwanzo*

**97. Kwa nini bendera ina nyota 50?***

- *kwa sababu kuna nyota moja kwa kila jimbo*
- *kwa sababu kila nyota kinawakilisha jimbo moja*
- *kwa sababu kuna majimbo 50*

**98. Jina la wimbo wa taifa ni lipi?**

- *The Star-Spangled Banner*

**C: Likizo**

**99. Ni lini tunasherehekea Siku ya Uhuru?***

- *Julai 4*

**100. Taja likizo mbili za Marekani.**

- *Siku ya kwanza ya mwaka mpya*
- *Siku ya Martin Luther King, Jr.*
- *Siku ya Marais*
- *Siku ya Kumbukumbu*
- *Siku ya Uhuru*
- *Siku ya Wafanyakazi*
- *Siku ya Columbus*
- *Siku ya Mashujaa*
- *Siku ya Shukrani*
- *Krismasi*

* Ikiwa una miaka 65 au zaidi na umekuwa mkaazi halali wa kudumu wa Marekani kwa miaka 20 au zaidi, unaweza kusoma maswali yaliyo na alama tu.